**TANGAZO LA SERIKALI NA. 434 la Tarehe 17/6/2022**

## SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
## (SURA 288)

# SHERIA NDOGO

***(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89***

**SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI ZA MAZINGIRA) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA, 2022**

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Hifadhi za Mazingira) (Marekebisho) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2022, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka, 2020 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Marekebisho GN Na. 836 ya tarehe 2/10/2020

2. Marekebisho yamefanyika katika kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza maneno *"fedha zitakazobaki baada ya makato ya faini na gharama nyingine zitarejeshwa kwa mmiliki wa mifugo".*

3. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 6 (4) cha Sheria Ndogo kuu kwa kufuta maneno masaa ishirini na nne(24) na badala yake kusomeka masaa arobaini na nane (48)

4. Marekebisho yanafanyika katika Sheria Ndogo kuu kwa kuongeza maneno *"ya asili,*

***Tangazo la serikali na 434 (linaendelea)***

*inayomilikiwa na Halmashauri au iliyopandwa kwa maelekezo ya Halmashauri"* mara baada ya maneno au miti.

Lakiri ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano mkuu wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Mbeya uliofanyika mnamo tarehe…………Mwezi …………., 2022 na lakiri iliyogongwa na kushuhudiwa na:-

TRIPHONIA KISIGA,
*Kaimu Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

DORMOHAMED ISSA RAHMAT,
Meya
Halmashauri ya Jiji la Mbeya

NAKUBALI,

**L.S**

INNOCENTLUGHA BASHUNGWA (MB)
Waziri wa Nchi-Or-Tamisemi